

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:2460117
Fax: 255 - 022 – 2460117
e-mail: Secretary@psc.go.tz;
Website: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA UBUNGO PLAZA,
BARABARA YA MOROGORO,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**DKT. MWANJELWA KUFANYA ZIARA YA KIKAZI KATIKA MIKOA
YA MWANZA NA SIMIYU**

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb) anatarajia kuanza ziara ya kikazi katika Mikoa ya Mwanza na Simiyu mapema mwezi Oktoba kuangalia masuala ya kiutumishi katika Mikoa hiyo.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Bwana Nyakimura Muhoji akizungumza jijini Dar es Salaam kuhusu ziara hiyo amesema kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri atafuatana na Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma watatu ambao ni Waheshimiwa Balozi (Mstaafu) John M. Haule, Bibi Khadija Mohamed Mbarak na Alhaj Yahaya Mbila.

"Lengo la ziara hii ni kukutana na kuzungumza na Viongozi na Watumishi wa Umma, kubainisha changamoto, kusikiliza kero zilizopo na kuzipatia ufumbuzi ili kuboresha utendaji wa kazi, kuwawezesha Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu pamoja na Watumishi wa Umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija kwa kuzingatia Maadili, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo pamoja na Maelekezo halali yanayotolewa na Serikali".

Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa na Makamishna wa Tume watatembelea na kuzungumza na Viongozi na Watendaji wa ngazi mbalimbali na Watumishi katika Mikoa na Halmashauri zifuatazo: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa

Mwanza, Halmashauri za Wilaya na Mji Magu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu,
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

Imetolewa na:



Richard M. Cheyo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Tume ya Utumishi wa Umma,

DAR ES SALAAM.

26 Septemba, 2019